# MKATABA WA UPANGAJI

**MKATABA HUU WA UPANGAJI** umefanyika leo tarehe **01 January 2021**

**KATI YA**

**SAID ABEID MBAROUK** wa S. L. P. 25296, DAR ES SALAAM, (ambaye katika Mkataba huu ataitwa hapa "MWENYE ENEO") kwa upande mmoja

**NA**

**MILGO LOGISTICS COMPANY LTD** wa S.L.P. 76608 Dar es Salaam (ambaye katika Mkataba huu ataitwa **"MPANGAJI"** ) kwa upande wa pili

**KWA KUWA MWENYE ENEO** ni Mmiliki halali wa eneo lililopo katika **kiwanja Na. "35" Mtoni Area**, likiwa na hati ya Usajili **Namba 56388, Wilaya ya Temeke** Dar es salaam, ambalo katika mkataba huu litajulikana kama "**ENEO"** NA

**KWAKUWA MWENYE ENEO** anaridhia kumpangisha **MPANGAJI** ENEO hilo, kwa ajili ya kuhifadhi na kutengeneza gari zake, kwa kipindi cha **Miaka mitano (05)** kutoka tarehe ya 01/01/2021 na kwa kodi ya **shilingi Milioni Tatu (Tshs 3,000,000/=) tu** kwa mwezi na **MPANGAJI** nae anaridhia kupangishwa Eneo hilo kwa kipindi cha miaka mitano (05) kwa masharti kama yanavyoonekana hapa chini.

**<u>MAKUBALIANO HAYA YANASHUHUDIA YA KWAMBA</u>**

1. Mwenye Eneo anakubali kumpangisha Mpangaji na Mpangaji anakubali kupanga katika Eneo hilo kwa ajili ya kuhifadhi na kutengeneza gari zake kwa kipindi cha MIAKA MITANO (05) kuanzia tarehe 01/01/2021 hadi tarehe 31/12/2025 kwa kodi ya shilingi Milioni Tatu (Tshs 3,000,000/=) tu kwa mwezi.

2. Siku ya kuweka saini mkataba huu Mpangaji atalipa kwa Mwenye Eneo kiasi cha **Shilingi Milioni Kumi na Nane (Tshs 18,000,000/=)** ikiwa ni kodi ya **miezi sita (6).** Na bakio la kiasi cha Shilingi **Milioni Kumi na Nane (Tshs 18,000,000/=) tu** zitalipwa si zaidi miezi saba (7) kutoka tarehe ya kusaini mkataba huu, kwa ajili ya kuondoa utata fedha hizo zitalipwa si zaidi ya tarehe **31/07/2021.**

3. Endapo kwa hali yoyote ile **MPANGAJI** atashindwa kulipa bakio la kiasi cha **Shilingi Milioni Kumi na Nane (Tshs 18,000,000/=)** kwa **MWENYE ENEO** ndani ya tarehe 31/07/2021. Mwenye Eneo atamuongezea Mpangaji muda wa siku saba (7) kulipa fedha hizo. Endapo atashindwa, itakuwa ni taarifa rasmi ya Mpangaji kuhama katika Eneo hilo baada ya kumalizika kwa muda wake wa miezi sita (6) aliyolipia. Mwenye Eneo hatakuwa na wajibu wa kutoa taarifa zaidi kwa Mpangaji, na kwarnba atakuwa na haki ya kumpangisha Mpangaji mwengine katika eneo, mkataba ambao utaanza baada ya kumalizika kwa kipindi cha miezi sita (6)
4. Iwapo Mpangaji atakuwa ana nia ya kuendelea na upangaji atatakiwa

kutoa taarifa ya kuendelea na upangaji kwa Mwenye Eneo siku Arobaini na tano (45) kabla ya kumalizika kwa muda wa Mkataba huu.

5. **KATIKA MKATABA BUU MPANGAJI ANAAHIDI KWAMBA:-**

a) Atalipa bili za umerne na usafi wa mazingira bila kukosa.

b) Atatumia eneo hilo kwa madhumuni ya kuhifadhi na kutengeneza gari zake tu.

c) Hatampangisha mtu mwengine Eneo hilo

d) Hatafanyajambo lolote ambalo litaleta usumbufu kwa Mwenye Eneo na majirani.

e) Atamrulrusu Mwenye Eneo, wakati wa mchana kwa madhumuni ya ukaguzi, kuingia katika eneo hilo ilimradi awe anampa Mpangaji taarifa mapema.

f) Wakati wote atahakikisha kwamba anatunza mazingira ya eneo hilo, aidha lipo katika hali ya usafi wa kuridhisha pamoja na kulifanyia matengenezoy ukarabati mdogo mdogo.

g) Hataruhusiwa kufanya ujenzi wowote utakaobadilisha muonekano wa eneo hilo bila ya ruhusa ya maandishi kutoka kwa Mwenye Eneo.

h) Atatakiwa kufanya shughuli zake kwa kufuata kanuni na sheria za nchi, Mwenye Eneo hatahusika kwa namna yoyote ile iwapo Mpangaji atashikiliwa na kushitakiwa na vyombo vya Usalama kwa kukiuka kanuni na sheria za nchi.

i) Bila ya kuathiri rnasharti yaliyotajwa katika kifungu cha nne(4) tajwa hapo juu, iwapo ombi lake la kuendelea kupanga katika eneo hilo litakubaliwa, atatakiwa kulipa kodi ya kuendelea na upangaji siku kumi (10) kabla ya kuanza kwa mkataba mpya.

6. **NA MWENYE ENEO NAE ANAAHIDI KWAMBA :-**

7. Kwa muda wote ambao Mpangaji atakuwa anatimiza masharti yatokanayo na makubaliano haya atamruhusu kufanya shughuli zake bila ya usumbufu wa aina yoyote.

8. Mkataba huu ni wa miaka mitano (05) kuanzia tarehe 01/01/2021, kwa ajili ya kuondoa utata malipo ya kodi yatakua ni ya miezi sita (6), mkataba huu utamalizika tarehe *31/12/* 2025, hata hivyo muda wa Mkataba huu unaweza kuongezwa kwa kipindi chengine zaidi na kwa masharti yaliyomo katika mkataba huu au masharti yoyote yale alimradi tu pawe na makubaliano ya kimaandishi kati ya Mwenye Eneo na Mpangaji.

9. Mkataba huu umefungwa kwa mujibu wa sheria, upande wowote

utakaokiuka masharti ya mkataba na kuathiri haki za upande mwengine, upande utakaoathirika utakuwa na haki ya kufuata taratibu zilizoweka iii kupata nafuu anazostahili kwa rnujibu wa sheria.

10. Iwapo Mpangaji ataamua kuvunja Mkataba huu, Mwenye eneo hatawajibika kurudisha kodi iliyolipwa.

11. Endapo Mkataba baina ya Mpangaji na Mwenye Eneo utakuwa umevunjika au umemalizika na Iwapo wakati wa makabidhiano Mwenye eneo atagundua kuwepo kwa deni la umeme au uharibifu wowote, Mpangaji atalazimika kulipia deni hila au gharama za matengenezo hayo.

**KWA SHUHUDA na UTHIBITISHO** wa makubaliano haya wahusika wote wamethibitisha na kutia saini zao siku na kwa namna ifuatayo:-

**UMETIWA SAINI** hapa Dar es salaam )
na mtajwa **SAID ABEID MBAROUK** )
ambaye namfahamu binafsi leo )
tarehe 01 Mwezi Januari 2021 )
**Mbele Yangu**

**SAID A. MBAROUK**

**Jina** ............................................
**Sahihi**..........................................
**Sifa** ............................................

Umetiwa saini na kugongwa mhuri
Wa Milgo Logistics Co. limited
Hapa Dar es Salaam leo
Tarehe 01 mwezi Januari 2021

JINA........................ADEN IBRAHIM ABDI
CHEO........MKURUGENZI..................
SAHIHI..........................................

MILGO LOGISTICS LIMITED
P. O. Box 76608
DAR ES SALAAM

**Mbele Yangu**
**Jina** ....KASHINDYE THABIT......
**Sahihi**..........................................
**Sifa** ..........WAKILI..............

**Umeandaliwa na:**
Said A. Mbarouk
S.L.P 25296
Dar es Salaam